**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA


Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu:
026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
**40479 DODOMA**


***Unapojibu tafadhali taja:***
**Kumb. Na. CA.313/315/01/8**

**19 Novemba, 2025**

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P 1923
**41185 DODOMA.**

Yah: **WARAKA WA ELIMU NA 06 WA MWAKA 2025 KUHUSU KALENDA YA MIHULA YA MASOMO KWA SHULE ZA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI MWAKA 2026**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na idadi sahihi ya siku za masomo kwa mwaka kama mitaala inavyoelekeza, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa **Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari (Kidato cha I – IV) kwa mwaka wa masomo 2026**.

3. Ni muhimu kuzingatia utekelezaji wa Kalenda husika kama ilivyopangwa ili kuepuka changamoto ya kutokamilisha ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa wakati na hivyo kulazimika kuweka mipango ya ufundishaji na ujifunzaji inayowanyima watoto/wanafunzi fursa ya kupumzika na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii katika familia na jamii zao.

4. Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa mwaka 2026 ni kama ifuatavyo:

| MIHULA | KUFUNGUA MUHULA | LIKIZO FUPI | | KUFUNGA MUHULA | IDADI YA SIKU ZA MASOMO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | KUFUNGA | KUFUNGUA | | |
| Muhula I | 13/01/2026 | 27/03/2026 | 08/04/2026 | 05/06/2026 | 96 |
| Muhula II | 06/07/2026 | 04/09/2026 | 14/09/2026 | 04/12/2026 | 98 |
| **Jumla ya Siku za Masomo** | | | | | **194** |

**Tanbihi:** .

- Siku za Masomo kwa mwaka ni **194**.
- Mashindano ya UMITASHUMTA yatafanyika tarehe 05/06/2026 hadi 17/06/2026, na UMISSETA yatafanyika tarehe 18/06/2025 hadi 30/06/2026.

- Mashindano ya Michezo ya Shule za Msingi na Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSA) yatafanyika tarehe 12/8/2026 hadi 23/8/ 2026.
- Shule zote zilizopo Manispaa ya Morogoro zitafunga tarehe 7/8/2026 na kufungua tarehe 24/8/2026 ili kupisha Mashindano ya FEASSA yatakayofanyika Mkoani humo. Hivyo, shule hazitafungwa wakati wa likizo fupi ya mwezi Septemba, 2026.

5. Ninashukuru kwa ushirikiano wako.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Wilaya,
**TANZANIA BARA.**

**Katibu Mtendaji**, Baraza la Mitihani la Tanzania.